# CLASS 7 MID TERM 3 2021
# KISWAHILI

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Kauleni alikuwa __1__. Hii ni kutokana na ukweli kuwa alipata malezi mema kutoka kwa wazazi wake. __2__ umri wa miaka kumi na __3__, alijiunga na shule ya upili. Aliendelea vyema hadi pale __4__ katika kidato cha pili. Alijiingiza katika utumizi wa __5__ kulevya __6__ kulelewa vizuri. Alipokuwa __7__ adhabu, alijiwa na kumbukumbu ya jinsi bangi __8__ mara ya kwanza.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | **A.** danga la mwana | **B.** jinga la mwana | **C.** denge la mwana | **D.** bwege la toto |
| **2.** | **A.** Alipofika | **B.** Alipofikia | **C.** Alipofikisha | **D.** Alivyofikia |
| **3.** | **A.** nne | **B.** tano | **C.** tatu | **D.** sita |
| **4.** | **A.** alivyoingia | **B.** alipoingia | **C.** aliyeingia | **D.** alikoingia |
| **5.** | **A.** madawa za | **B.** dawa za | **C.** dawa ya | **D.** madawa ya |
| **6.** | **A.** licha ya | **B.** maadamu ya | **C.** minghairi ya | **D.** mbali na |
| **7.** | **A.** anafanya | **B.** amefanya | **C.** akifanya | **D.** atafanya |
| **8.** | **A.** ilimhangaisha | **B.** ingemhangaisha | **C.** ilivyomhangaisha | **D.** ikamhangaisha |

Alikumbuka vile alivyozoeshwa __9__ ile na __10__. Ilikuwa ajabu yaani __11__ yeye mwenyewe hakuweza __12__. Wakati mwingine alijikuta akicheka __13__. Bila kujua, Kauleni akawa ametumbukia katika __14__ ulevi. Ama kweli __15__.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **9.** | **A.** tabia | **B.** mwenendo | **C.** fuska | **D.** mwendo |
| **10.** | **A.** wenzangu | **B.** wenzako | **C.** wenzake | **D.** wenzetu |
| **11.** | **A.** shime | **B.** shani | **C.** shari | **D.** nuksi |
| **12.** | **A.** kujidhibiti | **B.** kujithibiti | **C.** kujizatiti | **D.** kujisaili |
| **13.** | **A.** hobelahobela | **B.** kindakindaki | **C.** ovyoovyo | **D.** kwikwikwi |
| **14.** | **A.** kilinge cha | **B.** lindiko la | **C.** kikoa cha | **D.** lindi la |

**15.** **A.** mchovya asali hachovyi mara moja   **B.** baada ya dhiki ni faraja
**C.** kilicho baharini kakingoje pwani   **D.** mchuma janga hula na wa kwao

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

**16.** Chagua kitenzi kilichoundwa kutokana na nomino.

A. Mvumilivu - Uvumilivu
B. Mwaminifu - Aminika
C. Mapishi - Pikika
D. Wacheshi - Ucheshi

**17.** ***Chagua methali inayoafikiana na maelezo yafuatayo:***

Wakati wa hatari mtu hutumia kitu ambacho kiko karibu naye si kilicho mbali.

A. Kikulacho ki nguoni mwako.
B. Hamadi kibindoni ni silaha mkononi.
C. Bahati ya mwenzio usilalie mlango wazi.
D. Kwendako mema hurudi mema.

**18.** ***Andika kwa wingi:***

Nyuki hukaa mzingani naye jana segani.

A. Nyuki hukaa mizingani nao majana masegani.
B. Nyuki hukaa mizingani nao jana segani.
C. Nyuki hukaa mzingani nao jana segani.
D. Nyuki hukaa mizingani nao majana segani.

**19.** Chagua sentensi iliyo katika hali ya wastani.

A. Majibwa yaliyavamia majizi yakayaangamiza.
B. Mbwa waliwavamia wezi wakawaangamiza.
C. Vijibwa vilivivamia vijizi vikaviangamiza.
D. Kijibwa kilikiangamiza kijizi kikakiangamiza.

**20.** Chagua sentensi yenye matumizi sahihi ya koloni.

A. Jumatatu ni tarehe: 4/11/2021.
B. Kaka yangu alikula vyakula: yaani sima, wali na nyama.
C. Nyote mnaweza kuondoka: akasema mwalimu.
D. Majimbo niliyoyatembelea ni haya: Embu, Mombasa, Nairobi na Nakuru.

**21.** ***Andika kwa usemi wa taarifa:***

"Mkicheza vizuri tutaishinda mechi hii," alisema.

A. Alisema mkicheza vizuri, tutaishinda mechi hii.
B. Alisema kuwa wangecheza vizuri, wangeishinda mechi hiyo.
C. Alisema kuwa mkicheza vizuri tutaishinda mechi hii.
D. Alisema, "mkicheza vizuri, tutaishinda mechi hii."

**22.** Chagua sentensi yenye kiashiria cha karibu.

A. Mawaidha haya ninayokueleza yahifadhi moyoni.
B. Karibu na nyumba ile kuna jengo jingine.
C. Mitungi hiyo aliyobeba haina maji.
D. Taifa huru halipaswi kuwa na ufisadi.

**23.** Chagua sentensi yenye **-ji-** ya hali.

A. Williams ni mchezaji hodari sana.
B. Jinywa la joka lile linauma.
C. Tujisifu baada ya kufua dafu.
D. Uimbaji wake unavutia.

**24.** Chagua sentensi yenye nomino dhahania.

A. Maulidi alikula wali mtamu.
B. Mwizi alipigwa na umati wa watu.
C. Ng'ombe wa shangazi alikunywa maji mengi.
D. Wote waliombwa wafanye kampeini za amani.

**25.** Mama Boi ana watoto watatu. Wa kwanza anaitwa Fanta. Wa pili anaitwa Cocacola. Je wa tatu ni nani?

A. Sprite
B. Krest
C. Stoney
D. Boi

**26.** Chagua sentensi yenye vivumishi.
A. Daktari hodari amewatibu wagonjwa kadhaa.
B. Jiji limepambwa kwa maua.
C. Anga imebadilika leo.
D. Mwandishi aliyeandika insha alituzwa.

**27.** Chagua jibu linaloonyesha aina za mashairi.
A. Mizani, tathmini.
B. Tarbia, lakabu.
C. Ukwapi, utao.
D. Tathlitha, tarbia.

**28.** Chagua jibu lenye maelezo sahihi.
A. Mshahara ni malipo kwa ajili ya kazi ya kila siku.
B. Fichuo ni malipo kwa kijana baada ya kutoka jandoni.
C. Riba ni mkopo ambao hautozwi fedha za ziada.
D. Arbuni ni sehemu ya bei anayopunguziwa mnunuzi wa bidhaa nyingi.

**29.** ***Kanusha:***
**Kiserema kilichochakaa kinatumika kulimia tena.**
A. Kiserema kisichochakaa kinatumika kulimia tena.
B. Kiserema kisichochakaa hakikutumika kulimia tena.
C. Kiserema kilichochakaa hakitatumiwa kulimia tena.
D. Kiserema kilichochakaa hakitumiki kulimia tena.

**30.** Chagua sentensi yenye kielezi cha mahali.
A. Watoto wangu nitawapenda milele.
B. Jua huzama wakati wa magharibi.
C. Gari zee halifai kuegeshwa barabarani.
D. Kwa nini mnafitiana kisirisiri.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mapaka 40.***

Mwili wa binadamu una viungo vingi mno mathalani <u>figo</u>, ini, moyo, mapafu na vinginevyo. Ni matumaini yangu kuwa unafahamu fika matumizi ya kila kiungo. Kazi ya moyo ni kusukuma damu. Damu hii hupitia kwenye mishipa. Mishipa ya damu mwilini ni muhimu sana. Ni ukweli usiopingika kuwa binadamu hawezi kuishi pasi na kuwepo kwa mishipa inayosafirisha damu mwilini. Mishipa mwilini ni sawa na barabara nchini. Baraste ni miundo msingi muhimu sana kata dola lolote. Hii ni kwa sababu barabara huwa nyenzo ya usafirishaji wa bidhaa kutoka eneo moja hadi jingine.

Je, umewahi kusikia taifa ambalo limepiga hatua kimaendeleo bila kuwa na barabara bora? Taifa kama letu linategemea kilimo kwa kiasi kikubwa. Asilimia themanini ya Wakenya inajihusisha na kilimo. Mazao ya kawaida kama pareto, kahawa, chai, pamba na <u>miwa hukuzwa katika maeneo mbalimbali ya nchi</u>. Zao kama la miwa hukuzwa katika kaunti za magharibi ya nchi na zile za pwani kwa wingi. Ni vizuri kutaja hapa kuwa hata kaunti zile zilizosalia hukuza miwa kwa kiwango cha chini sana.

Maadamu tumeona Wakenya ni wanasanaa, ni vyema nisema hapa kuwa kilimo ni tegemeo kubwa sio tu kwa uchumi wa nchi bali pia kwa wakulima wenyewe. Hata hivyo hatuwezi kufaidi kutokana na juhudi zetu ikiwa barabara zenyewe si nzuri. Tanabahi kuwa lazima mazao yafikishwe sokoni wakati ufaao na kwa jinsi ifaayo. Ikiwa hili halitafanyika uwezekano wa kuhasirika ni mkubwa sana. Hilo nalo litakuwa pigo kubwa sana kwa uchumi wa nchi yoyote ile.

Mazao lazima yafike sokoni kwa wakati ufaao. Barabara zikiwa na shida hili halitawezekana. Barabara mbaya hukwamiza usafiri na kuyachelewesha mazao kama maua ambayo huishia kunyauka.

<u>Mbali na</u> kusafirisha mazao, barabara pia hutumika katika usafirishaji wa watu na wanyama. Kuna sababu nyingi sana zinazosukuma binadamu kusafiri. Chukulia huduma za afya. <u>Hizi huhitaji kutadarakiwa kwa upesi la sivyo mwathiriwa anaweza kuaga dunia.</u>

Sitakuwa nimepiga chuku nikisema kuwa karibu barabara zote zinazopatikana nchini ziko katika hali ya kukatisha tamaa. Baadhi ya barabara zimepuuzwa kwa muda mrefu na kuishia kuwa mtego wa mauti. Uendeshaji wa magari katika barabara hizi huwa ni kama mchezo wa mwajificho na mauti. Madereva hulazimishwa kuendesha magari zigizagi ili kuyakwepa mashimo makubwa. Hiki ni kichocheo kikubwa cha vifo.

Nikimalizia, tuhakikishe kuwa barabara zote za zamani zimekarabatiwa upya. Ni kweli haiwezekani na si rahisi barabara zote zitengenezwe kwa wakati mmoja kwa sababu ya gharama ya juu. Hata hivyo zipo barabara kuu ambazo zinaweza kutadarakiwa ili kuboresha usafiri na kuchangia ustawi wa kiuchumi. Ni vyema tujue kuwa kila mmoja ana jukumu la kuhakikisha kuwa analipa ushuru ili serikali ipate fedha za kujengea barabara.

**31.** Kazi ya figo ni

A. kiungo kilichomo ndani ya mwili wa mnyama ambacho hutoa nyongo na kubadilisha glukosi kuwa glukojeni.

B. kiungo cha mwili wa binadamu, wanyama au ndege kinachofanya kazi ya kuchuja na kusafisha damu.

C. kiungo kilichoko sehemu ya kifua ambacho husukuma damu ili ienee mwilini.

D. kiungo kilicho kufuani mwa binadamu kinachotumika kwa kutolea hewa chafu na kuingiza hewa safi.

**32.** Ni kaunti gani zinazokuzwa miwa hapa nchini?

A. Kaunti za eneo la magharibi pekee.

B. Kaunti za eneo la pwani pekee.

C. Kaunti za maeneo ya magharibi na pwani pekee.

D. Kaunti zote za nchi.

**33.** Chagua kauli ya kweli kulingana na kifungu.

A. Wakenya wengi ni wakulima.

B. Asilimia ishirini ya wakenya hawajihusishi na kilimo.

C. Wakenya wachache sana hujishughulisha na kilimo.

D. Kilimo cha miwa humu nchini ni sawa katika kaunti zote humu nchini.

**34.** Anayeshiriki kilimo anaweza kuathirika ikiwa

A. mavuno yake yatakosa kufika sokoni kwa wakati ufaao na kwa jinsi ifaayo.

B. ataendelea kutegemea kilimo pekee.

C. akuze mimea ya aina moja bila kuchanganya,

D. mazao yake hayatatumia barabara ambazo zimesakafiwa.

**35.** <u>Mbali na</u> ina maana ya

A. mbali ya

B. kando ya

C. zaidi ya

D. tofauti ya

**36.** Ni methali gani inayojumuisha ujumbe wa kauli hii?

<u>Hizi huhitaji kutadarakiwa kwa upesi la sivyo mwathiriwa anaweza kuaga dunia.</u>

A. Mbogo mwendo pole ni windo rahisi la simba.

B. Simba mwenda pole ndiye mla nyama.

C. Chelewa chelewa utampata mwana si wako.

D. Mpiga ngumi ukuta huumiza mkono wake.

**37.** Ni wazi kuwa

A. barabara zote zinazopatikana hapa nchini ni mbovu.

B. takribani barabara zote hapa nchini ni mbovu

C. barabara chache humu nchini ni za kukatisha tamaa.

D. hakuna barabara yoyote iliyo katika hali duni

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**38.** Muwa hukuzwa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Shamba la miwa huitwaje?
A. Bustani
B. Miche
C. Charo
D. Chalo

**39.** Kwa nini magari huendeshwa zigizagi?
A. Ni haraka ya kutaka kukusanya pesa nyingi.
B. Madereva wengi huendesha magari wakiwa walevi.
C. Madereva hujaribu kuyakwepa mashimo yanayopatikana katika barabara.
D. Huwa ni njia ya kuonyesha ubabe.

**40.** Kikwazo kikubwa cha usafiri bora kulingana na aya ya mwisho ni
A. upana wa barabara.
B. ulegevu wa madereva.
C. ukosefu wa hela.
D. kutowajibika kwa wote.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.***

Hata wa leo, siwezi kukuelezea kwa nini Robi walimfuata mzee yule. Alikuwa mzee aliyekuwa na maneno matamu ambayo humtoa nyoka pangoni. Kwangu nafikiria mzee huyu aliutumia ulimi wake wa kulazia kuwazaini akina Robi. Mzee Kwasi alikuwa tajiri mkubwa sana aliyemiliki mashangingi ainati. Alipenda sana kujiendesha licha ya kuwa alikuwa na pesa za kutosha za kumkodisha dereva. Inawezekana kuwa Robi na wenzake walivutiwa pia na gari lake.

Ajabu ni kuwa Robi na wenzake watatu walikubaliana na maneno ya Mzee Kwasi na moja kwa moja wakaingia katika shangingi lake. Wote walifululiza moja kwa moja mpaka katika mji karibu wa Dhuru. Hawakuwa wameuzuru mji huo hapo awali. Gari lilitiwa ufunguo na kuingia uchochoro wa kitongoji duni. Hapo sasa Robi na wenzake wakafungwa barakoa nyusoni. Wakawa vipofu wenye macho. Hawakujua walikokuwa wakipelekwa. Maskini watoto kumbe kwa kuingia garini wakawa wamejipalia makaa.

Baada ya muda kidogo walifika katika kijumba kidogo ambacho kilikuwa na mwangaza hafifu. Pale walipokezwa kwa wanaume ambao hawakuonekana kwa sababu ya uhafifu wa mwangaza wa chumba kile. Hivyo basi pasi na kupoteza wakati, waliongozwa katika chumba kimoja kilichokuwa na magodoro yenye maki ndogo ajabu na wakaambiwa walale. Wakati huu wote hawangejua walikuwa wapi maadamu ulikuwa usiku. Walimaizi kuwa asubuhi wangepewa mapokezi ya kukata na shoka.

Asubuhi ya majogoo waliamshwa haraka haraka na kuingizwa katika gari jingine tofauti na lililowaleta. Lilikuwa gari jeusi lenye madirisha kiwi. Baada ya saa mbili za safari, Robi na wenzake walifika mji mwingine ambao hawakuufahamu. Hapo walilakiwa na watu wanne wenye chuma ambao waliwahamishia katika gari jingine. Mmoja wa watu wale alibaki nyuma kidogo na kuwapokeza mkoba wenzake kwa kazi njema. Robi kuona hivyo waliingiwa na kiwewe. Hawakuwa na mwao kuwa walikuwa wametekwa nyara. Hapo ya wahenga yakatiwa kuwa jambo usilolijua ni sawa na usiku wa kiza. Robi alianza kujutia vitendo vyao.

Hatima yao iliishia nchi ya mbali. Huko walifanyishwa kazi za shokoa katika mashamba ya matunda. Hawakuamini kazi waliyoahidiwa ya donge nono ingegeuka na kuwa ya kuwalimia na kuwachunia maua wenye navyo kwa mshahara akali. Maadamu hawakujua jinsi ya kurejea nyumbani, walihiari kufanya kazi wakitafuta mbinu za kujinusuru.

Robi na wenzake walinyimwa nafasi ya kuwasiliana na jamaa zao. Nao ulinzi pale shambani ulikuwa wa kimataifa. Ilikuwa vigumu sana kupata usaidizi wowote ule. Pesa walizozipata ingawa zilikuwa kiduchu waliamua kuzihifadhi ili siku moja zingewafaa. Hata wahenga walisema akiba si mbi ingawa ya kumbi, siku ya kivumbi hutiwa motoni.

Akili ni nywele kila mtu ana zake. Mpango wao ulipoiva waliamua kumtumia mjakazi wa huko nyumbani kwa tajiri wao. Walimpa hela chache angaa aweza kulainisha moyo wake. Jioni ilipowadia, walitoka polepole kupitia mlango wa nyuma. Walielekea katika kituo cha polisi kilichokuwa karibu. Polisi nao walipopata habari waliivamia nyumba ile na kuwatia nguvuni wote waliokuwapo na kuwatia kuzuizini. Robi na wenzao

wakasafirishwa hadi nyumbani. Hata hivyo walionywa dhidi ya kuvutiwa na uzuri wa nje wa chochote wakionavyo.

**41.** Ulimi wa kulazia ni
A. kutumia nguvu za ulimi.
B. kutumia ulimi kudanganya.
C. kutumia ulimi ili mtu alale.
D. kutumia ulimi kuwavutia watu.

**42.** Kifungu kinaonyesha kuwa
A. Robi na wenziwe walilazimishwa kuandamana na Mzee Kwasi.
B. Robi na wenziwe waliyaamini maneno ya Mzee Kwasi na hivyo wakamfuata.
C. Robi na wenzake walikuwa na habari ya yale yaliyokuwa mbele yao.
D. Robi na wenzake walifahamishwa kuwa yote ambayo yangetokea hivyo hawakuwa na wasiwasi wowote.

**43.** Robi walifungwa barakoa nyusoni ili
A. wasiingiwe na vumbi machoni.
B. wasiweze kujulikana na watu wa mji wa Dhuru.
C. wasielewe walikokuwa wala walikokuwa wakielekezwa.
D. walale kutokana na uchovu mwingi wa safari.

**44.** Wamejipalia makaa ni tamathali gani ya lugha?
A. Nahau
B. Methali
C. Istiara
D. Tashbihi

**45.** Neno **'chuma'** limetumika katika kifungu. Lina maana gani?
A. Madini magumu.
B. Silaha hasa bastola ama bunduki.
C. Mtu mwenye nguvu nyingi.
D. Kuyatia matunda kikapuni.

**46.** Madirisha kiwi
A. humwezesha mtu aliye nje ya gari kumwona aliye ndani ya gari.
B. humwezesha aliye ndani ya gari na aliye nje ya gari kuonana.
C. humwezesha aliye ndani ya gari kumwona aliye nje ya gari bila ya yaye kuonekana.
D. hutumiwa na maadui kudhibiti kasi ya magari husika.

**47.** Robi na wenzake waliamshwa haraka haraka ili
A. kupata kiamshakinywa chao kikiwa moto.
B. waonyeshwe shughuli zilizowasubiri siku hiyo.
C. kuhamishwa kutoka sehemu hiyo ya mpito.
D. kulipwa mshahara wao wa siku zote walizokuwa kwenye safari.

**48.** Robi na wenzake
A. walilipwa kila siku.
B. walilipwa kila mwisho wa mwezi.
C. walipewa pesa zao kila wiki.
D. walipewa tu zawadi kwa kazi nzuri.

**49.** Chagua kauli isiyo ya kweli kulingana na aya ya mwisho.
A. Robi na wenzake waliamua kutoroka ili kujinusuru.
B. Robi na wenzake walikuwa na uhusiano mzuri na mjakazi.
C. Polisi walionyesha uwajibikaji wa hali ya juu kwa kufanya haraka kuwatia nguvuni.
D. Polisi waliwatia mbaroni wahusika wote na kuwapeleka kortini moja kwa moja.

**50.** Chagua methali mwafaka kuelezea kauli hii: Hata hivyo walionywa dhidi ya kuvutiwa na uzuri wa nje wa chochote wakionavyo.
A. Ashibaye hamjui mwenye njaa.
B. Asiyekuwapo na lake halipo.
C. Asiye na wake ana Mungu.
D. Chochote king'aacho si dhahabu.